# WIZARA YA KILIMO

# BODI YA KOROSHO TANZANIA

## MWONGOZO WA UPATIKANAJI WA KOROSHO GHAFI KWA WABANGUAJI WA NDANI KUPITIA SOKO LA AWALI KWA MSIMU WA 2021/2022

**Umetolewa na:-**
Bodi ya Korosho Tanzania,
S. L. P 533,
**MTWARA.**

**SEPTEMBA, 2021**

**MWONGOZO WA UPATIKANAJI WA KOROSHO GHAFI KWA WABANGUAJI WA NDANI KUPITIA SOKO LA AWALI KWA MSIMU WA 2021/2022**

## 1.0 UTANGULIZI

Kufuatia changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa malighafi kwa wabanguaji wa ndani kunakosababishwa na ushindani kutoka kwa wasafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi (*Exporters*), Serikali imeamua kuchukua hatua shirikishi za kuwezesha wenye viwanda vya ndani kupata malighafi. Hatua hizo ni pamoja na kuweka utaratibu utakaowawezesha wabanguaji wa ndani kununua korosho ghafi katika soko la awali. Soko la Awali katika zao la korosho ni mojawapo ya fursa kwa wabanguaji wa ndani kuweza kukabiliana na changamoto hiyo. Kwa mujibu wa Mwongozo huu wabanguaji wa ndani ndio watakaoruhusiwa kununua korosho ghafi katika soko la awali kwa kiasi cha kutosheleza mahitaji ya mwaka ya viwanda vyao vilivyopo hapa nchini.

## 2.0 MADHUMUNI

Madhumuni ya Mwongozo huu ni kuweka utaratibu utakaowawezesha wabanguaji wa ndani kupata korosho kwa ajili ya viwanda vyao vya ndani. Pia, masharti yanayopaswa kuzingatiwa ili kuhakikisha kuwa korosho zinazonunuliwa kwa utaratibu huu zinabanguliwa hapa nchini.

## 3.0 FAIDA ZA KUBANGUA KOROSHO NCHINI

Faida za kubangua korosho nchini ni pamoja na:-

i. Ongezeko la fursa za ajira hasa kwa akina mama na vijana zitokanazo na ubanguaji wa korosho nchini;
ii. Ongezeko la thamani ya mauzo ya korosho nje ya nchi;
iii. Ongezeko la biashara ya bidhaa mbalimbali zitokanazo na korosho badala ya kutegemea korosho ghafi. Bidhaa nyingine zinazoweza kuzalishwa na kuuzwa ni pamoja na sharubati (*juice*), mvinyo (wine), chachandu (pickle), maziwa, siagi (butter) jamu (jam), kashata, mafuta ya ganda la korosho (*Cashewnut Shell Liquid*), husks, n.k;
iv. Kupanua wigo wa soko la korosho iliyobanguliwa na isiyobanguliwa nchini;
v. Kutangaza nembo (*Brand*) ya korosho za Tanzania katika masoko ya Kimataifa; na
vi. Ongezeko la wawekezaji katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho nchini.

## 4.0 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA SOKO LA AWALI KATIKA ZAO LA KOROSHO NCHINI

Utaratibu wa uuzaji wa korosho katika Soko la Awali nchini unahusisha upatikanaji wa vibali vya ununuzi, mfumo wa uuzaji, udhibiti wa ubora wa korosho, utaratibu wa malipo, usafirishaji na utoaji wa taarifa.

### 4.1 Upatikanaji wa Leseni na Vibali

i. Mbanguaji ataomba leseni ya kununua korosho kwa ajili ya kubangua **(Buying License for Local Processing)** ndani ya nchi kupitia mfumo wa kieletroniki ulioko chini ya Wizara ya Kilimo (online through Agricultural Trade Management Information System under the Ministry of Agriculture - www.atmis.kilimo.go.tz) akiainisha mahitaji ya korosho ghafi ya kiwanda chake kwa mwaka nzima;

ii. Bodi ya Korosho itafanya tathmini ya maombi ya mbanguaji husika ili kujiridhisha uwezo wa kiwanda hicho;

iii. Bodi ya Korosho itafunga mkataba wa kisheria na Mbanguaji wa ndani;

iv. Bodi ya Korosho itatoa leseni kwa Mbanguaji na kuitaarifu Halmashauri anayotaka kununua korosho kwa ajili ya taratibu za usimamizi na utoaji wa taarifa za mwenendo wa mauzo; na

v. Endapo Halmashauri itaitaarifu Bodi kuwepo kwa mbanguaji anayekiuka taratibu za ununuzi wa korosho kupitia Soko la awali, Bodi itasitisha leseni kwa mbanguaji husika;

### 4.2 Utaratibu wa Uuzaji

i. Uuzaji wa korosho katika Soko la awali (*Primary Market*) utaanza mwezi Septemba na utaenda sambamba na uuzaji wa korosho katika soko la upili (*Secondary market)* kupitia minada itakayoendeshwa na Vyama Vikuu vya Ushirika hadi hapo viwanda vya ndani vitakapopata malighafi kulingana na maombi yao;

ii. Wakulima kupitia AMCOS watakuwa na hiari ya kuuza korosho katika Soko la Awali au soko la Upili;

iii. Bei ya korosho katika Soko la Awali ni ile itakayokubalika baada ya mapatano (*Negotiations*) baina ya Mbanguaji na Mkulima kupitia Vyama vya Ushirika husika;

iv. Mkulima atakayekuwa tayari kuuza korosho katika Soko la Awali atakusanya na kuuza korosho zake kwa Mbanguaji kupitia AMCOS husika;

v. Mbanguaji atatakiwa kulipia korosho pamoja na ushuru wa Halmashauri (*Crop cess*), ushuru wa Union, ushuru wa AMCOS, mchango wa pembejeo pamoja na gharama/tozo

nyingine zitakazokuwa zimeidhinishwa ikiwa ni pamoja na gharama za magunia kama hana ya kwake wakati wa utekelezaji; na

vi. Mbanguaji atatakiwa kubangua hapa nchini korosho zote atakazonunua kutoka kwenye Soko la Awali. Korosho zilizonunuliwa katika Soko la Awali hazitaruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi zikiwa ghafi kwa sababu yoyote ile.

**4.3 Uhakiki na Udhibiti wa Ubora wa Korosho katika Soko la Awali**

i. Uhakiki wa ubora wa korosho utazingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Ubora wa Korosho katika ngazi zote kama ulivyotolewa na Bodi ya Korosho katika msimu wa mwaka 2021/2022; na

ii. Uhakiki wa ubora wa korosho zitakazonunuliwa katika Soko la Awali utafanywa na Afisa Ugani wa Kijiji/Kata aliyeidhinishwa na Bodi ya Korosho Tanzania.

**4.4 Utaratibu wa Malipo**

i. Mbanguaji atatakiwa kulipia korosho alizonunua kabla ya kuzisafirisha ndani ya kipindi cha siku nne (4) baada ya makubaliano;

ii. Mbanguaji atatakiwa kukamilisha malipo ya korosho husika kupitia akaunti ya mkulima/AMCOS husika;

iii. Mbanguaji atatakiwa kulipa ushuru wa Halmashauri moja kwa moja kwenye akaunti ya Halmashauri baada ya kupewa namba ya malipo;

iv. Mbanguaji atatakiwa kutoa nakala ya nyaraka za malipo kwa AMCOS kama uthibitisho anapokwenda kuchukua korosho alizolipia; na

v. Mbanguaji hataruhusiwa kuondosha korosho katika AMCOS hadi mkulima atakapokiri kupata fedha zake zote za malipo kwa korosho husika.

**4.5 Usafirishaji**

i. Mbanguaji atatakiwa kuomba kibali cha kusafirisha korosho alizonunua katika Soko la Awali kutoka kwa Halmashauri akiwa ameambatisha nyaraka zinazothibitisha malipo ya korosho husika;

ii. Bodi ya Korosho itatoa kibali cha usafirishaji wa korosho kwa Mbanguaji husika baada ya kupata kibali kutoka Halmashauri kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji wa Hati za Kusafirisha Korosho; na

iii. Mbanguaji atatakiwa kuzingatia taratibu nyingine zote za usafirishaji wa korosho kama zilivyoainishwa katika Mwongozo wa Usimamizi wa Masoko uliotolewa na Bodi ya Korosho kwa msimu wa 2021/2022.

### 4.6 Utoaji wa Taarifa

i. Mbanguaji atawajibika kutoa taarifa ya ununuzi wa korosho kwa Halmashauri husika na Bodi ya Korosho kila wiki; na

ii. Bodi ya Korosho itatoa taarifa ya mauzo ya korosho ghafi katika Soko la Awali kipindi chote cha msimu.

## 5.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU

Ili kuhakikisha kuwa changamoto za uhaba wa malighafi kwa wabanguaji wa ndani zinapatiwa ufumbuzi, majukumu ya kiutendaji na kitaasisi yamegawanywa katika makundi mbalimbali ya wadau kama ilivyoelezwa hapo chini.

### 5.1 Wizara ya Kilimo

Katika kuhakikisha kuwa wabanguaji wa ndani wanapata malighafi ya kutosha, Wizara ya Kilimo itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya upatikanaji wa korosho kwa viwanda vya ndani; na

ii. Kuunganisha wadau wa Tasnia ya Korosho nchini katika kufikia malengo ya kuongeza thamani na masoko ya korosho inayozalishwa nchini.

### 5.2 Wizara ya Viwanda na Biashara

Wizara ya Viwanda na Biashara itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya kubangua korosho nchini; na

ii. Kuunganisha jitihada za wabanguaji katika kutafuta masoko ya korosho iliyobanguliwa pamoja na bidhaa zake.

### 5.3 Bodi ya Korosho Tanzania

Bodi ya Korosho ndiyo msimamizi mkuu wa mifumo ya uuzaji wa korosho nchini. Kutokanana nafasi hiyo Bodi ya Korosho itakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kusajili wabanguaji wote wa korosho nchini;

ii. Kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za ubanguaji wa korosho nchini;

iii. Kuanisha mahitaji ya korosho ghafi kwa wabanguaji wa ndani kwa kushirikiana na Umoja wa Wabanguaji Wakubwa na Wadogo wa Korosho;

iv. Kukagua viwanda vya kubangua korosho nchini;

v. Kufunga mkataba na mnunuzi (Mbanguaji) wa korosho kupitia soko la awali;
vi. Kutoa leseni ya ubanguaji wa korosho nchini;
vii. Kutoa leseni ya ununuzi wa korosho kutoka kwenye Soko la Awali;
viii. Kutoa vibali vya usafirishaji wa korosho iliyobanguliwa pamoja na bidhaa zake kwenda masoko ya nje (*Export*);
ix. Kuratibu vikao vyote vinavyohusu ubanguaji na upatikanaji wa malighafi kwa wabanguaji wa ndani;
x. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya zoezi la uuzaji na ununuzi wa korosho ghafi kupitia mfumo wa Soko la Awali;
xi. Kutunza kumbukumbu za AMCOS zilizouza korosho katika Soko la Awali;
xii. Kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bodi ya Korosho kutoa hati za kusafirisha korosho ghafi kwa wabanguaji wa ndani.
xiii. Kuhamasisha ubanguaji na ulaji wa korosho hapa nchini.
xiv. Kupokea malalalamiko/kero za wakulima na wadau wengine muhimu zinazotokana na utekelezaji wa Soko la Awali na kuzipatia ufumbuzi;
xv. Kusuluhisha migogoro ya ubora wa korosho katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na Soko la Awali; na
xvi. Kuchukua hatua za kisheria kwa wabanguaji watakaokiuka Mwongozo huu;

### 5.4 Sekretarieti za Mikoa

Ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na usimamizi wa kutosha katika ngazi ya Mikoa inayozalisha korosho nchini, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kusimamia na kufuatilia zoezi la uuzaji wa korosho katika Soko la Awali;
ii. Kufuatilia malalamiko/kero za wakulima na wabanguaji katika utekelezaji wa Soko la Awali; na
iii. Kuchukua hatua za kisheria kwa yoyote atakayebainika kukiuka taratibu za utekelezaji wa Soko la Awali kwa mujibu wa Mwongozo huu;
iv. Kuhamasisha wakulima kubangua korosho zao kupitia vikundi au mkulima mmoja - mmoja;

### 5.5 Ofisi za Wakuu wa Wilaya

Ofisi za Wakuu wa Wilaya zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuhamasisha wakulima kubangua korosho zao kupitia vikundi au mkulima mmoja mmoja;
ii. Kupokea taarifa za mahitaji ya malighafi kwa wabanguaji wa ndani katika wilaya husika kutoka Bodi ya Korosho;
iii. Kusimamia uuzaji na ununuzi wa korosho katika Soko la Awali;
iv. Kuhakikisha kuwa kila mkulima aliyeuza korosho katika Soko la Awali anapata malipo aliyostahili na kwa wakati;
v. Kuhakikisha kila mbanguaji aliyenunua korosho kutoka kwenye Soko la Awali anabangua hapa nchini;
vi. Kupokea malalamiko/kero za wakulima na wengine wanaohusika katika utekelezaji wa Soko la Awali na kuzipatia ufumbuzi; na
vii. Kuchukua hatua za kisheria kwa yoyote atakayebainika kukiuka taratibu za utekelezaji wa Soko la Awali katika uuzaji wa korosho nchini.

### 5.6 Halmashauri za Wilaya

Ili kuwa na ufanisi wa kutosha, Wakurugenzi wa Halmashauri zinazozalisha korosho nchini watakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuwasiliana na AMCOS ambazo wakulima wameridhia kuuza korosho zao katika Soko la Awali;
ii. Kutoa vibali vya usafirishaji wa korosho kupitia Soko la Awali kwa wabanguaji wa ndani;
iii. Kuandaa ratiba ya ununuzi wa korosho ghafi katika soko la awali;
iv. Kuwezesha Maafisa Ugani wa vijiji/kata kusimamia ubora wa korosho zinazonunuliwa katika Soko la Awali; na
v. Kufuatilia zoezi la uuzaji na ununuzi wa korosho kutoka kwenye Soko la Awali pamoja na kutoa taarifa za mwenendo wa mauzo ya korosho katika Soko la Awali.

### 5.7 Tume ya Maendeleo ya Ushirika

i. Kusimamia AMCOS na UNION ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia mwongozo huu; na

ii. Kuchukua hatua za kisheria kwa Chama kitakachobainika kukiuka taratibu za utekelezaji wa Soko la Awali kwa mujibu wa Mwongozo huu;

### 5.8 Chama Kikuu cha Ushirika (*Union*)

i. Kuainisha AMCOS zinazotekeleza Soko la Awali katika msimu husika;
ii. Kusambaza magunia na kamba kwenye AMCOS zinazotekeleza Soko la Awali;
iii. Kufuatilia mwenendo wa mauzo ya korosho katika Soko la Awali; na
iv. Kunapokuwa na ushindani wa bei katika Soko la Upili kushirikiana na AMCOS katika kuhakikisha kuwa wabanguaji wa ndani wanapata malighafi ya kutosha.

### 5.9 Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS)

i. Kuratibu kikao cha mapatano/makubaliano ya bei kati ya mbanguaji na wakulima wanaotaka kuuza korosho katika Soko la Awali;
ii. Kusimamia utekelezaji wa bei ya korosho itakayokubaliwa na wakulima katika Soko la Awali;
iii. Kuhakikisha kuwa korosho zitakazouzwa na wakulima katika Soko la Awali zinakidhi viwango vya ubora unaohitajika na mbanguaji husika;
iv. Kukusanya tozo mbalimbali zinazostahili ikiwa ni pamoja na ushuru wa AMCOS, ushuru wa Halmashauri, ushuru wa Union, gharama ya magunia na kulipa kwa wahusika kwa wakati unaostahili;
v. Kuhakikisha kuwa malipo kwa wakulima wanaouza katika Soko la Awali yanafanyika kwa wakati unaostahili; na
vi. Kutoa taarifa kwa wakati kwa Mkuu wa Wilaya na Bodi ya Korosho juu ya ukiukwaji wowote wa taratibu za Soko la Awali kwa mujibu wa Mwongozo huu.

### 5.10 Mbanguaji wa Ndani

i. Kuainisha mahitaji ya korosho ghafi na kuwasilisha kwa Bodi ya Korosho na Halmashauri anayotaka kununua korosho;
ii. Kuwasilisha maombi ya leseni ya kununua korosho ghafi kutoka kwenye Soko la Awali kwa Bodi ya Korosho akiainisha Halmashauri atakazonunua korosho;
iii. Kusaini mkataba wa ununuaji wa korosho katika soko la awali baina yake na Bodi ya Korosho;
iv. Kushirikiana na Umoja wa Wabanguaji Wakubwa au Wadogo katika ununuzi wa korosho ghafi na upatikanaji wa masoko ya korosho zilizobanguliwa ndani na nje ya nchi;

v. Kuwasilisha taarifa mbalimbali za utekelezaji wa mpango huu kwa Bodi ya Korosho Tanzania;

vi. Kubangua korosho zote atakazonunua kutoka kwenye Soko la Awali;

vii. Kuzingatia gharama za uzalishaji wa korosho ghafi ikiwa ni pamoja na faida kwa mkulima/wakulima husika wakati wa mapatano ya bei ya kununulia korosho kutoka kwenye Soko la Awali; na

viii. Kutunza kumbukumbu za malipo aliyoyafanya kwa korosho alizonunua kutoka kwenye AMCOS husika.

### 5.11 Umoja wa Wabanguaji wa Korosho nchini TACP na UWWKT

Umoja wa wabunguaji wa korosho nchini utakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kusimamia na kuhakikisha kwamba korosho zinazonunuliwa kupitia Soko la Awali zinabanguliwa hapa nchini;

ii. Kutoa taarifa ya mwenendo wa ubanguaji wa korosho nchini kila mwezi kwa Bodi ya Korosho;

iii. Kutoa taarifa Bodi ya Korosho/Halmashauri za Wilaya juu ya changamoto zozote zinazojitokeza katika utekelezaji wa mpango huu na mapendekezo ya namna ya kuzitatua changamoto hizo; na

iv. Kutoa taarifa kwa mamlaka husika pale inapotokea ukiukwaji wowote wa taratibu miongoni mwa wanachama wa TACP au UWWKT.

### 5.12 Mkulima

i. Kuwa na hiari ya kuuza korosho ghafi kwenye Soko la Awali;

ii. Kuvuna korosho na kupanga katika madaraja kabla ya kupeleka katika AMCOS kwa ajili ya uuzaji;

iii. Kushiriki kikao cha kukubaliana bei ya kuuzia korosho na Mbanguaji husika katika Soko la Awali;

iv. Kuwa na akaunti benki kwa ajili ya kupokelea malipo ya korosho;

v. Kuepuka kuchanganya korosho na vitu visivyo korosho ikiwa ni pamoja na korosho zilizoharibika;

vi. Kuzingatia gharama za uzalishaji wa korosho wakati wa mapatano ya bei ya kuuzia korosho kwa Mbanguaji ili kukubaliana bei inayompatia faida mkulima; na

vii. Kutoa taarifa kwa mamlaka husika pale inapotokea ukiukwaji wowote wa taratibu za mwongozo huu.

**5.13 Taasisi za Fedha (Mabenki)**

i. Kutoa huduma za fedha kwa wakulima na wabanguaji ili waweze kufikia malengo yao;
ii. Kuhamasisha wakulima na wabanguaji kutumia huduma za kibenki; na
iii. Kuwatembelea na kuwafungulia wakulima akaunti kwa ajili ya kupokelea malipo ya korosho.

## 6.0 MAKOSA NA ADHABU

i. **Kununua korosho kwenye Soko la Awali bila kibali.** Korosho husika zitataifishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni za Mwaka 2010.
ii. **Kuchelewa kufanya malipo kwa mkulima.** Mkulima kupitia AMCOS husika anaruhusiwa kuuza kwa mbanguaji mwingine au Soko la Upili (Mnada). Sambamba na hili; mbanguaji husika atazuiwa kununua korosho kutoka kwenye Soko la Awali kwa kipindi cha msimu mzima.
iii. **Kusafirisha korosho ghafi zilizonunuliwa kwenye Soko la Awali kwenda masoko ya nje ya nchi.** 100% ya thamani ya korosho husika italipwa na mbanguaji husika kwa Bodi ya Korosho ikiwa ni sambamba na mbanguaji kuzuiwa kununua korosho kutoka kwenye Soko la Awali kwa kipindi cha msimu mzima.

## 7.0 HITIMISHO

### 7.1 Wajibu wa Pamoja

i. Kuhakikisha kuwa madhumuni na utekelezaji wa Mwongozo huu yanazingatia sera na sheria za nchi;
ii. Kutoa taarifa mapema kuhusu suala lolote litakaloathiri utekelezaji wa Soko la Awali.
iii. Kuhakikisha Soko la Awali linakuwa na manufaa kwa wadau wote kuanzia wakulima hadi wabanguaji.
iv. Kuhakikisha kila mdau anatimiza wajibu wake kwa mujibu wa Mwongozo huu.
v. Kushirikiana katika eneo lolote linalofanikisha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya ndani;

### 7.2 Muda wa Utekelezaji

Utekelezaji wa Mwongozo huu ni kuanzia tarehe 01 Septemba 2021 hadi 30 Agosti 2022.

### 7.3 Ilani

Serikali haitawajibika kwa namna yoyote ile kwa mdau/mhusika ambaye hatazingatia utaratibu uliowekwa katika Mwongozo huu.

### 7.4 Mwisho

Mwongozo huu unasomwa sambamba na Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009, Kanuni zake za Mwaka 2010 pamoja na Miongozo mingine itakayotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania.

Mwongozo huu umetolewa leo tarehe 30 AGOSTI, 2021

..................................

Francis Alfred

**KAIMU MKURUGENZI MKUU**